



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



TANGAZO KWA UMMA

Mafunzo ya Usimamizi wa Ghala

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoungwa kwa Sheria Namba 10 ya Mwaka 2005 na marekebisho yake chini ya Sheria Namba 4 Sura ya 339 R.E. 2016. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) cha Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inapenda kuwajulisha waombaji leseni na wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuwa imeandaa mafunzo ya wafanyakazi wa ghala wapya, yanayotarajia kuanza tarehe **24 hadi 27 Julai 2024** katika **Ukumbi wa ofisi za Bodi (WRRB) zilizopo Mtaa wa Nyerere jijini Dodoma.**

Mafunzo haya yanalenga wafanyakazi watano kisheria ghalani, ambao hawakuwahi kupata mafunzo na mitihani inayotolewa na Bodi. Aidha, wadau wengine wenye nia ya kujifunza shughuli za usimamizi wa ghala kama vile Wakurugenzi wa kampuni za Waendesha Ghala, wanunuzi na wengine wote wanakaribishwa. Mafunzo haya yatahitimishwa kwa mtihani pamoja na vyeti kwa watakaofaulu.

Mafunzo yatakayotolewa ni kwa ajili ya kuelekea Msimu wa mbaazi na dengi kwa Mwaka 2024/2025. Gharama za mafunzo kwa mhusika mmoja ni shilingi laki saba hamsini elfu tu (750,000/=). Mwisho wa kufanya malipo ya mafunzo hayo ni tarehe 23 Julai 2024, wasiofanya malipo kwenye muda huo hawatapokelewa.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Bi Grace Raphael kwa simu namba 0713387482 au kwa barua pepe grace.raaphael@wrrb.go.tz

Imetolewa na

Mkurugenzi Mtendaji
19 Julai, 2024